

Mvuvi Joseph Sichilima akinadai samaki aina ya sangara kwa wafanyabiashara katika soko la samaki lililopo Kijiji cha Kasanga mwambao wa Ziwa Tanganyika wilayani Kalambo, Rukwa.

**Na Peti Siyame**

# Soko la Kasanga neema mpya ya wavuvi Rukwa

KUPITIA Bandari ya Mpulungu, shughuli za kibiashara zinatazamiwa kuimarika na hivyo uchumi wa wakazi wa Kata ya Kasanga na wilaya ya nzima ya Kalambo mkoani Rukwa unategemewa kupanda pia.

Hii ni kutokana na kuanza kwa shughuli za soko la kisasa la samaki lililopo Kata ya Kasanga katika mwambao mwa Ziwa Tanganyika wilayani Kalambo baada ya kusimama kwa miaka minane tangu ujenzi wake ulipokamilika na soko kuzinduliwa mwaka 2012.

Sasa soko hilo linatarajiwa kuwawezesha wavuvi na wafanyabiashara kuwa na eneo salama la kuuzia mazao ya samaki na kupata taarifa za bei ya masoko.

Katika mahojiano na mwandishi wa makala haya, wavuvi kadhaa wameeleza furaha yao kutokana na soko hilo kuanza kutumika rasmi baada ya kusubiri kwa muda mrefu.

Wavuvi hao wanasema kukosekana kwa soko hilo, kulisababisha wafanyabiashara wa samaki kutoka nchi jirani ya Zambia kunufaika zaidi lakini sasa kupitia soko hilo, watanzania watanufaika ipasavyo.

"Kwa muda mrefu wavuvi tulikuwa tukitumikishwa na wamiliki wa makampuni ya uvuvi yaliyopo katika Mji wa Mpulungu mwambao mwa Ziwa Tanganyika upande wa Zambia," anasema mvuvi Joseph Sichilima.

Anazidi kufafanua: "Walikuwa wakitupatia maboti ya uvuvi, injini, mafuta na zana bora za uvuvi na tukishavua lazima tukawauzie lakini kwa bei wanayopanga wenyewe... tulitumikishwa kama watumwa."



Wanawake wajasiriamali wakikata samaki aina sangara kwa ajili ya wateja wao baada ya kuanza kwa shughuli rasmi katika soko la samaki la Kasanga. (Picha zote na Peti Siyame).

Kauli yake hiyo inaungwa mkono na wavuvi wengine wakiwemo John Sikazwe na John Chifunda wakisema kuanza kwa soko hilo ambalo wafanyabiashara kutoka Zambia watalazimika kuja kununua kwa bei ya soko kunatarajiwa kuwakomboa.

Furaha yao imekolezwa na kauli ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, Palela Msongela alipozungumza nao sokoni hapo na kuwapatia miezi miwili ya kufanya shughuli zao bila kulipia ushuru.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, wavuvi wakishavua samaki wabichi watakuwa wakiwahifadhi katika chumba cha barafu kabla ya kuwauza kwa wajasiriamali wanawake ambao ndio watawauzia wateja.

Anafafanua kwamba kutakuwa pia na minada mitatu itakayofanyika sokoni hapo kila Jumapili, Jumanne na Alhamisi .

Hata hivyo, changamoto kubwa ambazo bado zinalikabili soko hilo ni kukosa chumba kinachohifadhi ubaridi mkali chenye uwezo wa kugandisha samaki kwa dakika chini ya 30.

Mkurugenzi anataja changamoto nyingine kwamba ni soko hufikiwa na maji pindi maji ziwani yanapokuwa mengi wakati wa masika ambapo miundo mbinu iliyopo haiwezi kupitisha maji hayo na kuyamwaga umbali mrefu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Soko, Kennedy Sinyangwe anasema takribani watu 70,000 wanaoishi katika vijiji vinavyozunguka eneo hilo wanashughulika na uvuvi.

Anaongeza kwamba wastani wa tani 170,000 za samaki zinavuliwa kwa mwaka katika eneo hilo na kwamba changamoto kubwa iliyokuwepo ni kukosekana kwa soko la uhakika lenye ushindani, hali iliyosababisha nguvu za wavuvi kunyonywa na wafanyabiashara wachache.

Anasema soko hilo lina sehemu ya kuuzia samaki wabichi, kusafirishia na kukaushia na pia sehemu ya kuuzia na kuhifadhia samaki wakavu.

Kadhalika kuna ofisi za utawala.

Ni soko ambalo limejengwa likiwalenga wavuvi na wafanyabishara wa ndani na nje ya nchi.

Soko hilo la samaki Kasanga lilijengwa na Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (Mviwata) kwa kushirikiana na Taasisi ya kimataifa isiyo ya kiserikali ya GRET.

Mshirika mwingine wa ujenzi alikuwa ni Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kabla ya kugawanywa na kuanzishwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo kupitia mradi wa masoko ya ujumla ya mazao katika mikoa ya Mbeya na Rukwa.

Ujenzi wake ulianza Desemba 2009 na kukamika Novemba 2011 ambao sehemu ya gharama ya ujenzi zinazofikia Sh 802,488,528 kwa sehemu kubwa zilitolewa na Jumuiya ya Ulaya (EU).

Ujenzi ulisimamiwa na mshauri elekezi, kampuni ya ITECO Consult ya Morogoro huku wakandarasi wakiwa Kwizombe, Leadcom na Chex (JV) kutoka Dodoma.

Mchanganuo wake ulikuwa ni ufadhili wa Jumuiya ya Ulaya Sh 493,931,500, mchango wa MVIWATA Sh 166,500,000, GRET ilichangia Sh 49,931,500 na Halmashauri za Wilaya ya Sumbawanga na Mbalali kwa pamoja zilichangia Sh 138,750,000.

Wakazi wa vijiji jirani na soko hilo kupitia mtandao wao walichangia nguvu kazi kwa kushiriki kazi mbalimbali na kwa hiyari yao pia walitoa kiwanja katika eneo lililojengwa soko.

Soko hili lilifunguliwa rasmi na aliyekuwa Makamu wa Rais, Dk Mohamed Gharib Bilal, Februari 23, 2012.

Changamoto zilizosababisha soko lisifanye kazi kwa miaka minane ni pamoja na kutokuwepo kwa nishati ya umeme katika majengo ya soko.

Changamoto nyingine iliyosababisha shughuli kushindwa kuanza sokoni hapo ni kutokuwepo kwa majokofu ya kuhifadhia samaki ambayo ni mahitaji muhimu.

Scanned by CamScanner

a. Hata
li, daktari
a kabla
na nini,"

hivi sasa
mia vizuri
upatikanaji

wa sheria
na Bunge
ya wazee
alieleza

ba serikali
usafiri wa
nia (ATCL).
hizo kwa
Tunaomba
hie usafiri
aalumu na
Mbonde.
wa Baraza
Mwenyekiti
a Dar es
aliwataka
ka kuwa

**MWENYEKITI wa Baraza la Wazee wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mohammed Mtulia, akihutubia Baraza la Wazee wa la Kata ya Vingunguti, wakati wa hafla ya uzinduzi wa mfuko wa baraza hilo, Dar es Salaam, juzi.** (Picha na Christopher Lissa).

# Wavuvi Kalambo waagizwa kutumia soko la samaki

**Na JANE MWAKYOMA,** *Kalambo*

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo mkoani Rukwa, Msongela Palela, amewataka wavuvi kuacha kuuza samaki ndani ya maji na badala yake watumie soko la samaki la Kasanga.

Soko hilo, lillilojengwa maalumu kwa kuuzia samaki hao ili kukuza kipato chao na nchi kwa ujumla.

Akizungumza na wavuvi hao baada ya kutembelea soko la samaki la Kasanga, alisema wavuvi wanaovua upande wa Tanzania hawana budi kuacha tabia ya kuuzia samaki majini na badala yake wapeleke katika soko hilo.

"Niwatake wavuvi wote kuleta samaki hapa, kwani miundombinu ya umeme barafu na vichanja imeboreshwa na wanunuzi wapo kwa wingi tofauti na hapo awali ambapo ilikuwa inawalazimu kupeleka samaki kwenye soko la Mpulungu nchini Zambia,"alisema.

Alisema utaratibu uliopo, wavuvi wakivua samaki watakuwa wakihifadhiwa katika chumba cha barafu kabla ya kuwauza kwa wajasiliamali wanawake, ambao watawauzia wateja wengine na kutakuwa na minada mitatu itakayofanyika sokoni hapo kila Jumapili, Jumanne na Alhamisi ili kuwasaidia wavuvi kukuza kipato chao.

Msongela alisema ingawa bado soko hilo lina changamoto ndogo ndogo, lakini wavuvi wanatakiwa kutumia fursa ya kufunguliwa kwa soko kuu la Kasanga kwa ajili ya kuongeza vipato vyao.

Kwa upande wao wavuvi hao, walisema zaidi ya miaka nane walikuwa wakitumikishwa na wamiliki wa kampuni za wavuvi zilizopo katika Mji wa Mpulungu mwambao mwa ziwa Tanganyika, upande wa Zambia, ambapo walikuwa wakipewa boti ya uvuvi na zana bora za uvuvi.

"Kwa zaidi ya miaka minane, sisi wavuvi tulikuwa tunatumikishwa na wamiliki wa kampuni za wavuvi zilizopo katika mji wa Mpulungu mwambao mwa ziwa Tanganyika upande wa Zambia, walikuwa wakitupatia maboti ya uvuvi, injini, mafuta na zana bora za uvuvi, sasa ukivua lazima tukawauzie lakini kwa bei wanayopanga wenyewe,"walisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Soko, Kenedy Sinyangwe, alisema takribani watu 70,000 wanaoishi katika vijiji vinavyozunguka eneo hilo, wanashughulika na uvuvi na wastani wa tani 170,000 za samaki zinazovuliwa kwa mwaka.

**Uwezeshaji**

**SOKO LA SAMAKI**

Wavuvi wilayani Kalambo wametakiwa kuacha kuuza samaki ndani ya maji na badala yake watumie soko la samaki la Kasanga.

Scanned by CamScanner